

MWISHO NI UWINGU

Valentine Ndege
Mugumu-Serengeti
05.09.2019

Moderato

0758 084 222

Soprano/Alto

1.* Ta a i me zi mi - ka ka ma m shu ma a u wa
*Ma cho na ya fu mbu a la ki ni - si o ni cho

Tenor/Bass

S./A.

1.* ka o na lo - gi za la ma u ti li me ta - nda
*cho te nu ru i ng'a a yo i me fi - fi - a

T./B.

S./A.

1.*Na fu ngu a ki nywa ni se me ma ne no ha ya to ki u -
*Mba li ndu gu m me so ge a m ki wa ni me ba ki nda -

T./B.

S./A.

1.*li mi m - zi to kwe li - mwi - sho ni - u
ni ya je - ne za kwe li - mwi - sho ni - u

T./B.

1

Mwisho ni Uwingu

S./A.

T./B.

1.

2.

wi ngu

wi ngu.

O
R
G
A
N

2. *Fahari za dunia, naondoka nyuma naziacha, si fedha heshima wala dha-habu,
 *Si nyumba wala gari, nitakwenda navyo kaburini, si cheo, wazazi wala majirani:
 *Jeuri yangu imekwisha, hakika du-nia ni mti mkavu: Kweli mwisho ni Uwingu
 *Duniani tunasafiri, makao ya milele mbinguni kwa Baba: Kweli mwisho ni Uwingu.

3. *Futeni ye' machozi, nyamazeni msinililie, kwani sote tupo sa-fa-rini,
 *Mnapo ona haya, jiulizeni ninyi wenyewe, safari ni heri au mmelala:
 *Muwe watu wanyenyekevu, tubuni na kusali bi-la kuchoka: Kweli mwisho ni Uwingu
 *Nitazame mara ya mwisho, nilivyo lala usingizi wa maisha: Kweli mwisho ni Uwingu.

4. *Njiani miiba mingi, safari ya kwenda mbinguni, hofu na hatari nyingi zakazana,
 *Milima na mabonde, mawimbi na misukosuko, tumaini la safari laffia:
 *Msiishi usingizini, safari ya mbinguni iwakute macho: Kweli mwisho ni Uwingu
 *Acha mambo ya duniani, vumilia jizuie 'tapata uzima: Kweli mwisho ni Uwingu.

5. *Kitabu cha hukumu, naona kimefunuliwa, nisomewe mema pia ma-baya,
 *Tafakari nzi-to, yanitengenezea taswira, ya matendo yangu huko duniani:
 *Kama niliyatenda mema, hukumu nitashinda mbingu kuingia: Kweli mwisho ni Uwingu
 *Kama nilitenda mabaya, hakika nitatupwa kwe' shimo la moto: Kweli mwisho ni Uwingu.

6. *Kwaheri baba yangu, ndugu jamaa na majirani, kwaheri mama kwaherini rafiki,
 *Hakika nilitoka, uchi tumboni mwa mama yangu, uchi ninarudi tumboni mwa nchi:
 *Nifunikeni kwa udongo, mwenyewe nibakie ndani ya kaburi: Kweli mwisho ni Uwingu
 *Sala zenu pia maombi, salama zinifikishe Paradisoni: Kweli mwisho ni Uwingu.